**IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH**

**(E.ISSN: 2805-413X) (P.ISSN: 2992-247X )** *Dkt. Kawira Kamwara, **

https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 12 || December, 2024 ||*

Ulinganifu na Ulinganuzi wa Kimtindo katika Ujenzi wa Upembezwaji wa Mwanamke katika Bunilizi Tuele za Clara Momanyi na Omar Babu

# Ulinganifu na Ulinganuzi wa Kimtindo katika Ujenzi wa Upembezwaji wa Mwanamke katika Bunilizi Tuele za Clara Momanyi na Omar Babu

***Dkt. Kawira Kamwara,***

***Mount Kenya University***

**IKISIRI**

Jamii nyingi za Kiafrika humpembeza mwanamke kwa kumweka katika ngazi za chini huku mwanamume akiwekwa kwenye ngazi za chuni.. Upembezwaji wa mwanamke katika tungo za kifasihi na katika maendeleo ya jamii ni matokeo ya mwingiliano wa fahamu tambuzi na fahamu bwete za mtunzi hasa kwa mujibu wa utamaduni wa jamii lengwa. Mwingiliano huu wa ufahamu tambuzi na ufahamu bwete unaekezwa kwa makusudi katika utunzi wa tungo mahususi kama ilivyo kwenye tungo za Momanyi 'Ngome ya Nafsi'katika *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004), *Tumaini* (2006) na *Nakuruto* (2010) nazo za Babu ni *Kala Tufaha* (2007), *Heri Subira* (2010) na 'Ndoa ya Samani' (2011. Data ya usomi huu ilitokana na usomaji wa bunilizi hizi maktabani. Tuliweza vilevile kutumia mitandao kurutubisha utafiti wetu. Hatimaye, ilichambuliwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Hivyo, ni kwa jinsi gani watunzi Momanyi na Babu wanarandana kimitindo katika ujenzi wa maudhui ya upembezwaji wa mwanamke kisanii katika jamii? Je, kuna naman ambavto wanatofautiana katika ususi wa kazi zao? Ni vipi ambavyo mwanamke anapembezwa kiutunzi katika kazi teule? Maswali haya ndiyo tulipania kuyajibu katika makala haya.

**Isitilahi maalumu-*Ujitambuzinafsia, Upembezwaji, Mitindo, bunilizi***

## Utangulizi

Kila mtunzi huzingatia mtindo wake binafsi katika kukuza kazi yake ya kisanaa. Hivyo, utafiti huu umejikita kuchunguza namna ambavyo waandishi Momanyi na Babu wanavyosuka kwazi zao na kubaini namana ambavyo wanafanana pamoja na kutofautiana kimtindo kwenye tungo zao teule.katika kushughulikia suala hii, tutaangazia mazingira yao ya utunzi pamoja na jinsi wanavyowasawiri wahusika wao ili kukuza maudhui ya ujenzi wa ujitambuzinafsia na upembezwaji wa mwanamke katika kazi zao. Uchanganuzi wote utafanywa kwa mujibu wa mhimili ya nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ambayo ndiyo dira tuliyoteua ya kuongoza utafiti huu.

## Mtazamo wa Kinadharia

Uhakiki huu umeongozwa na nadharia ya Ufeministi. Nadharia hii hulenga kuangazia masuala ya kijinsia katika jamii. Ni dhana inayopinga mielekeo ya mfumo wa ubabedume. Ni nadharia iliyoasisiwa na Wollstonecraft (1792) katika makala yake yaliyotetea ujenzi wa utambuzi wa jamii usiobagua wanajamii kwa misingi ya jinsia. Nadharia ya Ufeministi inaungwa mkono na Beauvoir (1949), anaposhambulia jamii kwa jinsi inavyojenga ujitambuzi hasi wa jinsia kwa kumpembeza mwanamke kupitia misingi ya asasi kama ndoa na utamaduni. Kwa kupitia

mtazamo wa Beauvoir, utamaduni unaozingatiwa na jamii una nguvu ya aina fulani inayotumiwa kama kigezo cha kuiongoza.

Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999), wakimnukuu Eagleton (1991), nadharia hii huwa na matapo manne, mojawapo likiwa ni tapo la Ufeministi wa Kiafrika. Tapo hili huonyesha nia na malengo kuhusu hali halisi katika jamii za Kiafrika. Kulingana na hoja hii, nadharia hii itatuongaza kuchunguza masuala ya kijinsia katika kazi teule ili kuafiki mielekeo ya kijamii kuhusu ujenzi wa ujitambuzi nafsia wa jinsia. Uhalisia wa maisha ya jamii ya watunzi utaweza kubainika kupitia kwa usawiri wa wahusika pamoja na mjukumu yoa. Vilevile, tutachunguza masuala ya kijinsia katika kubainisha hatua za ujenzi wa jamii mpya ambayo wanajamii wathaminiwa bila ubaguzi. Kauli hii itatusaidia kubaini ni kwa jinsi gani Momanyi anaangazia suala la upembezwaji wa mwanamke katika jamii. Hivyo, nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ndiyo imetumika katika kuhakiki suala hili.

## Ulinganifu wa Usawiri wa Wahusika Katika Kukuza Maudhui ya Upembezwaji wa Mwanamke Kati ya Bunilizi za Clara Momanyi na za Omar Babu

Katika kukuza maudhui ya ujenzi wa ujitambuzinafsia wa jinsia, waandishi Momanyi na Babu wamepiga hatua nzuri kwa kugusia mambo yanayomwathiri mwanamke katika jamii. Wawili hawa wamebainisha kuwa, mwanamke anajengewa ujitambuzinafsia hasi kupitia mfumo wa ubabedume, mila na desturi za utamaduni jadi na asasi za kijamii zikiwemo ndoa za mapema, ubaguzi wa kimasomo na kimya cha kulazimishwa. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inatambua kwamba, mwanamke anapembezwa kupitia asasi za kijamii tulizotaja. Hoja hii inabainika katika Kimani (2003) akimnukuu Ogundipe Leslie (1994) anaposema kuwa, mwanamke wa Kiafrika anapembezwa kwa njia nyingi na ndiye binafsi, mwenye uwezo wa kupigania uhuru na haki yake.

Momanyi katika kuwasawiri wahusika Naseko katika 'Ngome ya Nafsi' (2004) na Tumaini katika *Tumaini* (2017), amefaulu kuonyesha jinsi mwanamke anavyojengewa ujitambuzinafsia hasi kwa kupangiwa ndoa za mapema. Mzee Masumbuko babake Tumaini, anakwenda Maunguja kumtafutia Tumaini mume. Naseko naye, ananyanyuliwa juujuu na vijana na kupelekwa kwa lazima kwa mzee wa rika la babake. Momanyi amefaulu kuonyesha kuwa, mwanamke ametambua dhuluma anazopitia katika jamii na kujitolea kubadilisha hali yake. Hii ni kupitia kwa jitihada za wahusika Tumaini na Naseko kutoroka na kujiokoa kutoka kwenye hali dhalimu zinazowakumba. Ujitambuzinafsia hasi wanaojengewa unabadilishwa na ujasiri wao wa kujiokoa wao wenyewe. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inamhimiza mwanamke atumie uwezo wake na ujasiri ili aweze kuibuka na ushindi. Tumaini anatorokea kwa mamake mdogo na kutimiza ndoto yake ya kuwa daktari. Naseko naye, anatorokea kwa BiTesi ambako anapata mazingira bora ya kuendeleza masomo yake.

Kwa upande mwingine Babu (2010), anamsawiri mhusika Sabra kama shujaa asiyekuwa tayari kupembezwa na kujengewa ujitambuzinafsia hasi katika ndoa dhalilishi. Anajikuta kwenye ndoa ya kupangiwa na babake ambayo inamletea huzuni moyoni. Baada ya kuteseka mikononi mwa

Khalid, anatoroka na kuomba Khalid ampe talaka yake. Sabra anamwomba Khalid talaka na anapoipata, anajitafutia mwanamume kufu yake ambaye anamwoa na kumheshimu. Kupitia ndoa ya Sabra ya chuo cha pili, Babu anaonyesha kwamba, wanaume wote si wabaya. Wapo wanaomjengea mwanamke ujitambuzinafsia chanya kama anavyofanya Heri, mume wa pili wa Sabra. Nadharia ya Ufemisti wa Kiafrika inapiga vita asasi kandamizi kwa mwanamke. Babu anaunga mkono hoja hii kwa kuonyesha ufanisi wa Sabra baada ya kuamua kumwacha Khalid kwa kumpembeza na kumvunjia heshima yake kama mwanamke na binadamu mwenzake.

Katika kuangazia upembezwaji wa mwanamke kielimu, Momanyi (2006) amefaulu kuyaweka wazi masaibu ya mtoto msichana kupitia uhafidhina wa baba yake mzazi. Tunaelezwa kuwa babake Mzee Masumbuko, hathamini masomo ya mtoto msichana. Kwake yeye, anamtaka tu atimize ada za upashwaji tohara na kuolewa bali si kuendeleza masomo yake. Kimani na Njogu (1999) wanasema kuwa, fasihi inafaa itumike kama jukwaa la kueleza changamoto anazopitia mwanamke katika ulimwengu uliotawaliwa na ubabedume na kuonyesha njia za kukabiliana nazo.

Momanyi anaangazia jinsi babake Tumaini anamhangaisha Tumaini kwa kusema, *Tuma ... Tuma hatakuwa msungo ... hakuna mtoto wa kike asiyepashwa tohara katika mlango huu…*(uk. 39-40).Ingawa huu ndio msimamo wa Mzee Masumbuko kuhusu msichana, tunaona kwamba jamii imehamasishwa kuhusu vita dhidi ya mila kandamizi. Jamaa yake yenyewe inaungana na Tumaini kupigania haki ya masomo yake. Momanyi amefaulu kuonyesha jinsi mila potovu zinavyopigwa vita katika jamii kama anavyopendekeza Steady(1981). Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inatambua haja ya kupiga vita mila na desturi dhalilishi kwa mwanamke.

Hivyo, Momanyi amefaulu kuonyesha kuwa desturi zinazomjengea mwanamke ujitambuzinafsia hasi zinapigwa vita. Mtoto msichana anatambua haki yake na kuipigania. Mbali na mhusika Tumaini, Momanyi anamsawiri mhusika Naseko katika ‘Ngome ya Nafsi’ kama mtu ambaye anapembezwa kwa kunyimwa nafasi ya kuendeleza masomo yake. Tunaona jinsi Naseko anavyotaka kuozwa kwa lazima akiwa bado mdogo. Momanyi anaangazia ubinafsi wa mwanamume katika jitihada za kufuata mila na itikadi za utamaduni jadi. Ingawa Naseko anafungiwa katika chumba cha Mzee Sakaja, anatumia ujasiri na ujanja wake kutoroka. Kauli hii inaungwa mkono na nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kwamba, ni mwanamke pekee anayeweza kupambana na upembezwaji wake na kupigania haki zake katika jamii. Katika hali ya kushughulikia suala la upembezwaji kimasomo, Babu amefeli kudhihirisha uwezo wa mwanamke wa kujikomboa kisaikolojia na kupigania nafasi yake stahiki katika jamii.

Babu anaibua taswira ya uwezo kamili wa utamaduni na ubabedume juu ya mwanamke katika bunilizi zake tulizoteua. Kufuatia jinsi anavyomsawiri mhusika Kibibi katika *Kala Tufaha* (2007), Babu anaonyesha athari za mafunzo ya dini ya Kiislamu (na ambayo wanume wanayatumia kama kisingizio cha kumpembeza mwanamke), kwa mtoto msichana hasa kuhusu utiifu kwa wazazi. Wahusika wake wasichana hawapingi maoni ya wazazi wao kuhusu maisha yao binafsi.

> ‘Mzee aliamua nisisome zaidi,’ alijibu Kibibi. ‘Lakini hata ningesoma, kuna faida gani katika masomo ya mwanamke? Mwisho wake kuolewa na kisha kuwa mke nyumbani. Tutafanyaje na ndivyo jamii yetu ilivyo?’ (uk. 33-34).

Kupitia kwa kauli hii, mwandishi anaashiria utamaushi wa mwanamke. Ni kiumbe dhaifu na hivyo, anazingatia na kufuata mkondo wa ada  za jadi utamaduni wa jamii yake. Taswira anayotuchorea Babu ni kinyume na wito wa wanaufeministi wanaosema kwamba mwanamke anahitajiwa kupinga upembezwaji sio kuhisi kuwa yu dhaifu kwa sababu ya maumbile yake. Kibibi anaikubali hali hii kwa sababu ndivyo jamii yake ilivyomlea na kumrenga. Ndoto yake ya kusoma na kuwa daktari imedidimizwa kabisa. Ndipo tunaweza kudai kwamba, mwandishi huyu anakubaliana na mchango wa malezi kwa mtoto anapokua.

Kuhusu kigezo cha ufisadi kinavyochangia upembezwaji wa mwanamke, waandishi Babu na Momanyi wamefaulu kuonyesha kuwa, mwanamke ana uwezo wa kupigania haki zake. Ingawa mwanamume anatumia nafasi na mamlaka aliyopewa na jamii  kumjengea ujitambuzinafsia hasi, mwanamke anaweza kutumia akili yake kujikomboa. Nadharia ya Ufeministi inatambua uwezo wa mwanamke wa kupigana na udhalilishwaji wake na kujipatia hadhi katika jamii. Kupitia mhusika Tumaini, tunaona jinsi babake anavyokula yamini kumkatizia masomo yake. Anampa chifu Andrea hongo ili aliondoe jina la Tumaini kwenye orodha ya wafadhiliwa wa kimasomo. Bi. Selina anasema, '*Babako alikuja kumshawishi chifu ahakikishe wewe huko katika orodha ya hao watakaofadhiliwa*' (uk. 97*).*

Ukweli ni kwamba chifu huyu anafaulu kuliondoa jina la Tumaini kwenye orodha hiyo. Japokuwa hivyo, Momanyi anaonyesha jinsi mwanamke anavyopigania nafasi yake kwa kumsawiri Tumaini kama msichana jasiri anayevamia kikao cha D.O na kutetea haki yake. Momanyi anafaulu kuonyesha kuwa, mwanamke anaweza kupigania anachotaka maishani kama inavyopendekezwa na wanaufemisti waliokwisha tajwa. Ujasiri huu wa Tumaini unamfanya apate ufadhili na kuendeleza masomo yake licha ya babake kuapa hatosoma.

Fauka ya hayo, Mzee Masumbuko anamhonga chifu kwa mbuzi ili asimchukulie hatua katika juhudi za kumwoza Tumaini kisiri. Tunasoma,

> Chifu huyo kitimba kwira pia alichukua mlungula kutoka kwa wanakijiji ili aweze kutekeleza mambo fulani kwa kutumia cheo chake… alimwona Mzee huyu akimkokota mbuzi kuelekea uani mwa chifu Andrea…(uk. 54-55).

Kwa kuangazia ufisadi wa chifu Andrea, Momanyi anafichua maovu anayotendewa mwanamke kwa ushirikiano wa viongozi walafi. Lakini, tunaona kuwa serikali inakashifu kitendo hiki kupitia kwa onyo analopewa chifu Andrea na D.O. wa tarafa hii.. *Anaonywa kukomesha tabia hiyo la sivyo, angepoteza wadhifa wake* (uk. 104). Momanyi amefaulu kuonyesha jinsi vita dhidi ya upembezwaji wa mwanamke vinaungwa mkono na serikali ili kuhakikisha kuwa, mwanamke anapata haki zake katika jamii zinazozingatia utamaduni jadi katika mfumo wa Ki-Ubabedume. Hata hivyo, mapambano yangali yanaendelezwa kwani taasubi za kiume zina makali yake katika jitihada za kuendeleza dhuluma hizo anuwai dhidi ya mwanamke. Hii ni kwa sababu jamii bado inaendeleza dhuluma hizi kwa msimamo wa kutimiza mila na desturi za utamaduni jadi. Lakini tunaona jitihada wazi na za kutia moyo upande wa serikali katika kupambana kuona kuwa mwanamke anafurahia haki ya masom  sawia na mwanamume.

Kwa upande wa Babu, yeye anamtumia mhusika Kibibi kubainisha jinsi mwanamke anavyopigania haki yake baada ya kubakwa na Fumbwe. Kibibi anahisi kwamba, ni lazima Fumbwe angewajibikia kitendo chake. Anamtafuta wakili Neema ambaye anahakikisha kwamba,

uchunguzi wa chembechembe za damu umefanyika na kuthibitishwa kuwa, mtoto wa Kibibi ni wa Fumbwe na hivyo, kumwezesha mwanamke kupigania nafasi yake bila kufa moyo. Hii ni kwa sababu Fumbwe anamhonga wakili wa kwanza Kidawa, anayejiondoa kwenye kesi ya Kibibi. Kinyume na Kidawa , wakili Neema anakataa hongo na anamtetea Kibibi kwa uwezo wake wote. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inatambua muungano wa wanawake kama kundi linalodhulumiwa na kutetea haki zao. Uwezo wa wanawake wanapoungana, zinamfanya Fumbwe ashindwe kuingilia uchunguzi wa chembechembe za damu unaofanyiwa Ulaya. Mwandishi anasema,

> 'Pesa ilivunja nguu na milima ikalala… wa kwanza nilimweka sawa. Shilingi elfu hamsini zilitosha kumrubuni, akajiondoa kwenye kesi… Haikuwezekana?'…. (uk. 103).

Babu amefaulu kubainisha kuwa, ingawa mwanamke anaweza kukosa pesa za kumlipa wakili, bado anaweza kupata haki yake. Pamoja na ufisadi wa Fumbwe, ukweli anaopigana kuupinga unapatikana. Babu anapenya nafsi ya mwanamke na kuonyesha uwezo wake wa kupigania ujitambuzinafsia wake chanya baada ya kujitambua na kukielewa kile anachokitaka na maishani mwake. Babu anatumia ujielewaji na ujitambuzi huu wa mwanamke kama kigezo cha kushinda vita dhidi ya upembezwaji.

Zaidi ya hayo, tunaona kwamba waandishi Momanyi na Babu wanawasawiri wahusika wa kiume ambao wanasimama kidete kumpembeza mwanamke. Hawa ni wahafidhina ambao kamwe hawabanduki kubadili mtazamo wao hasi kuwahusu mtoto msichana na mwanamke. Tabia yao ni ile ile ya kumtekeleza mwanamke pindi anapokwenda kinyume na matarajio yao. Hoja hii inaonyesha jinsi Momanyi na Babu wameshindwa kubadili mtazamo wa jamii na hasa kuwahusu wanaume wahafidhina ili kukumbatia mabadiliko na ufanisi wa jinsia ya kike katika jamii. Momanyi katika *Tumaini* (2007), anamsawiri Mzee Masumbuko kama mhafidhina sugu anayeshikilia mtazamo jadi katika kuwalea watoto wake na hasa wa kike. Hata baada ya kushauriwa na familia yake, bado anashikilia msimamo duni na hasi kumhusu mwanamke. Tunasoma,

> 'Nisikilizeni, kisha mnisikilize kwa makini. Mimi ni mtu na hamsini zangu. Sijashindwa kuwalea wanangu. Tuma… Tuma…(uk. 39).

Taswira inayoibuka kupitia dondoo hili ni kuwa, jamii itaendelea kubaki nyuma kimaendeleo ilmuradi haitapiga vita mila dhalimu kumhusu mwanamke. Mzee Masumbuko ni mwakilishi wa kizazi cha jadi kisichokumbatia mabadiliko katika jamii. Inaonekana bado kuna pengo kwa wanaharakati wa mrengo wa Ufeministi katika kuihamasisha jamii zaidi ili kuasi ada zinazomjengea mwanamke ujitambuzinafsia hasi. Ni kweli kuna kundi ambalo limekumbatia mabadiliko kama akina mama Halima na kwa kiasi, Mze Shabani. Lakini, jamii lazima iwe na matumaini kwamba, hali itabadilika na kumpa mwanamke nafasi stahiki zaidi. Bi Halima anasema,

> 'Mzee Masumbuko anajaribu kupigana na upepo wa mabadiliko … Mawe! … wakati huu tulio nao hakuna mzazi atakayemlazimu binti yake kutahiriwa' …(uk. 25).

Kwa hivyo, yapo matumaini kupiga vita mila dhalilishi zinakazotekelezwa na wazee kama Mzee Masumbuko. Hii itakuwa hatua kubwa kwa wanaufemisti katika kukomesha ada dhalilishi kwa

mwanamke. Kwa kuangazia kazi za Babu, tunaona maoni sawa na ya Momanyi kupitia unyama anauotenda Mwalimu Selemani kwa bintiye Kibibi. Mwalimu Selemani amesawiriwa kama mhusika mhafidhina anayeamini kwamba, kumsomesha mtoto msichana ni kumfunza ukahaba. Hii ndiyo sababu inayomfanya akatae kugharamia masomo ya Kibibi ya shule ya upili. Mwalimu Selemani anakosa kutambua uwezo wa mwanamke wa kujiendeleza kimasomo na kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya kijamii. Anaposhauriwa na mwalimu wa Kibibi ampeleke shule, Mwalimu Selemani anasema,

> ‘Nina uwezo wa kumlipia masomo binti yangu. Pesa ziko Alhamdulillahi! Kitu nisichokitaka ni huko kuendelea na masomo. Elimu atapata lakini mwisho wake ni nini? Kuolewa’… (uk. 29).

Babu ameshindwa katika kuangazia jinsi jamii inavyounga mkono na kushinikiza suala la kumpa mtoto msichana masomo. Hivyo, wito wa wanaharakati wa mrengo wa kiufeministi bado hauzingatiwi kikamilifu. Mwalimu Selemani ni mwakilishi wa kundi la wazee linalomjengea mwanamke ujitambuzinafsia hasi kwa kumhusisha na ukahaba ikiwa wataposoma. Hatua mwafaka na madhubuti zaidi zinahitaji kuchukuliwa ikiwa wazee kama Mwalimu Selemani watabadili nia na misimamoyao ya kijadi na hasi na kukumbatia maendeleo ya jinsia zote mbili katika jamii.

Bado jamii haijabadilika na kumtengea mwanamke majukumu stahiki. Ingali inashikilia mtazamo wa kijadi ya kwamba, mabinti ni watu wa kuolewa na kulea familia. Mtazamo kama huu unapingwa na Wamitilah (2002) anaposema kuwa, nadharia ya ufeministi wa kiafrika inapigania nafasi sawa za jinsia katika jamii.

**Ulinganuzi wa Usawiri wa Wahusika Katika Kukuza Maudhui ya Upembezwaji wa Mwanamke Kati ya Kazi za Clara Momanyi na Omar Babu**

Katika kuwasawiri wahusika wa kike, Babu ameonyesha athari za malezi katika msingi wa dini ya Kiislamu kwa mtoto msichana. Anaelekea kuipa kipau mbele dhana ya utiifu kwa wazazi jambo ambalo linayafinya mawazo yake na kukosa kujikomboa. Katika kuzingatia mawaidha ambayo yamejawa na ubinafsi kwa msingi wa taasubi za kiumbe, mwanamke anaathiri maisha yake kwa njia hasi. Katika maisha ya utotoni, tunampata mwanamke dhaifu asiye na ujitambuzinafsia na asiyetambua haki zake au jinsi ya kujipigania pindi anapokumbwa na changamoto maishani. Ni kama wahusika wake wa kike hasa wasichana wanajitolea mhanga kuwafurahisha wazazi kwa kuzingatia kaida za ubwete wa jamii lengwa. Wakereketwa wa mrengo wa ufeministi na wanaufeministi wanatambua uwezo wa mwanamke wa kupigania haki zake na kuishi bila kudhulumiwa. Hoja hii ni bainifu kupitia kwa mhusika Kibibi, ambaye anashindwa kupigania lengo lake katika maisha. Tunasoma,

> Hakutaka kupingana na wazazi wake. Alikuwa radhi kufanya lolote kuwaridhisha, ila tu la kumuasi Mola. Akiamini kwamba ni jukumu lake kuwatii wazazi wake...(uk. 28).

Kauli ya Kibibi inamwakilisha mtoto msichana aliyekolea na kuzama kwenye utiifu wa wazazi na mila na desturi za kurithiwa. Babu ameegemea sana kwenye mafunzo ya dini ya Kiislamu kuhusu wajibu na majukumu ya mtoto kwa wazazi wake. Anaonyesha nafasi ya dini katika kujenga hulka ya mja. Aidha, dini ya Kiislamu imetenga majukumu ya wanajamii kwa msingi wa kijinsia. Mwanamume anapaswa kuitunza familia huku mwanamuke akitimiza majukumu ya

kinyumbani (japo pia anaruhusiwa kufanya kazi nyingine ila mapato yanakuwa yake binafsi na wala hajukumishwi kutoa masrufu ya kifamilia). Babake Kibibi Mwalimu Selemani, anachukua mwelekeo kumhusu mwanamke kuwa hata akisoma, hatima yake ni kuolewa na kutimiza majukumu hayo tu ya kinyumbani. Anayadhibiti maisha ya bintiye kikamilifu. Anatumia mafunzo ya kidini kama kisingizio cha kumkandamiza mwanamke kwani hata jirani yake Mzee Majembe, anawapa watoto wake wa kike na kiume nafasi sawa za kupata elimu. Babu anamtumia Mwalimu Selemani kuwakilisha wanaume wenye tamaa ya mali kupitia ulipwaji wa mahari. Anaendeleza mfumo jadi kumhusu mwanamke. Wanaume kama hawa wangali katika lepe la jana katika kuzitambua na kuzitetea haki za mwanamke.

Kinyume na Babu, Momanyi anaangazia jamii iliyozinduka na kupata mwanga wa utambuzi wa haki za mtoto msichana na mwanamke na kuzipigania. Anaonyesha ushujaa wa mwanamke katika kupigania anachoona kinamfaa binafsi bila kujali hisia za wazazi wake. Mwanamke huyu tunampata kupitia kwa mhusika Tumaini katika *Tumaini* (2017). Anapopangiwa tohara ya kulazimishwa, anagura nyumbani kwao usiku wa manane na kupata makao kwa mamake mdogo. Anakataa kushirikishwa kwenye ada zilizopitwa na wakati. Anatambua uwezo alio nao wa kujiamulia mambo kuhusu maisha yake. Mamake anapomsihi akubali kupashwa tohara anamwambia, ‘ *Ikiwa unayotaka kunieleza yanahusu tohara, Mama Sahau. Sahau kabisa maana nilisema tangu kitambo kuwa mila hiyo ni ya kizamani, ni ya kikatili na kishenzi… kufanya hivyo ni sawa na kujichimbia kaburi…*(uk. 16-17).

Taswira tunayoipata kupitia msimamo wa Tumaini ni kuwa ni msichana jasiri na shujaa. Nadharia ya ufeministi wa Kiafrika inatambua kuwa, mwanamke anaweza kupigania haki yake na kujijengea ujitambuzinafsia chanya pindi anapojikomboa kimawazo na kutambua haki yake pamoja na malengo yake maishani. Momanyi anadhihirisha jinsi wanaharakati wa mrengo wa ufeministi wamepiga hatua kuwahamasisha wanawake kuhusu haki zao. Amefanikiwa pakubwa katika kuipenya nafsi ya mwanamke na kugundua uwezo wake wa kupigana dhidi ya upembezwaji wake ili kujipa nafasi stahiki katika jamii. Ni mwanamke anayetaka kubadili mkondo wa maisha yake kama anavyomwambia mhusika Sifa, ‘*I want to shape my destiny.’* Mwanamke amegundua ndiye mwenye uwezo huo binafsi ndipo aweze kujikomboa na kuishi bila kudhulumiwa.

Mbali na mhusika Kibibi katika *Kala Tufaha* (2007), Babu anaangazia udhaifu wa mwanamke katika *Heri Subira* (2010). Amesawiri hali na mazingira yanayoonyesha upofu wa mwanamke wa kuona maisha yake ya baadaye. Jambo hili linadhihirika kupitia kwa mhusika Sabra anayepangiwa aolewe na mwanamume asiyemjua. Sabra anakubali kuingia katika ndoa hiyo na anadhalilishwa kindoa na Khalid mumewe. Babu anazidi kuonyesha kwamba, mwanamke asipojipigania, ni vigumu kupata ukombozi wa kimwili na kimawazo. Babu ameshindwa kuelewa kuwa, mwanamke anahitaji kutimiziwa matakwa ya hisia za mapenzi na kupewa uhuru wa kujichagulia mchumba. Si Sabra pekee bali hata dada zake Shufaa na Nasra, wanaozwa wangali wadogo. Kinyume na upofu wa mwanamke katika kazi za Babu, Momanyi anaonyesha kwamba, mwanamke amepiga hatua katika kujijengea ujitambuzinafsia chanya katika jamii.

Momanyi amefaulu katika kuonyesha hatua ambazo jamii imepiga katika kuhakikisha kuwa mwanamke anajikomboa. Kupitia kwa mhusika Naseko, tunapata kumwona akitoroka kutoka

kwa Mzee Sakaja. Anatumia uwezo wa akili yake kujinasua kutoka kwa utamaduni kandamizi wa ndoa za mapema. Anapopata makao kwa Bi. Tesi, mwandishi anatueleza,

> …Aliwaza juu ya wale wasichana kama yeye ambao hawakubahatika kutoroka kama yeye. Aliwaona kama viumbe waliofungiwa ndani ya ngome, ngome za nafsi zao wenyewe….(Uk. 114).

Inabainika kuwa, iwapo Naseko anafanikiwa kutoroka, kuna wengine wanaokosa kujiokoa kama yeye. Hii ina maana kwamba bado pana haja kubwa ya kuihamasisha jamii kuukomesha upembezwaji wa mwanamke. Iwapo wasichana wengi wangelijitambua kama Naseko, hakungekosekana baadhi ya wale wanaoshindwa na kunaswa kwenye wavu wa ada kandamizi zinazomjengea mwanamke ujitambuzinafsia hasi. Ni muhimu kutaja kwamba, kunga ya taashira anayotumia Momanyi kurejelea wakati ambapo Naseko na Tumaini wanatoroka na kutoka katika mazingira kandamizi na kuyaendea yale yenye manufaa na yanayojali maslahi yao, kunampa uelewa wa jinsi mwanamke anavyoweza kuchukua hatua yeye binafsi, ili ajikomboe. Hatumwoni Babu akitumia kunga kama hiyo katika kuueleza utambuzi na utetezi wa haki za mwanamke na ujitambuzi wake chanya katika jamii zizo hizo zilizoloa utamaduni jadi na mfumo wa Ki-Ubabedume.

Momanyi amefaulu kubainisha hali ya mwanamke katika jamii pamoja na kuonyesha umuhimu wa ushirikiano wa jinsia ya kike ndipo mwanamke aweze kushiriki kwenye maendeleo ya jamii kikamilifu na bila kubaguliwa. Hoja hii inapendekezwa na Kimani na Njogu (1999) wanaposema kuwa, fasihi inafaa itumiwe kama jukwaa la kubainisha hali ya mwanamke kwa njia ya ufanisi na kuudhirisha waziwazi udhalimu anaotendewa mwanamke na njia za kuukomesha.

Kuna haja ya kupatikana hamasisho zaidi la kuwazindua wale wachache (kama anaowawazia Naseko), waliojifunga kwenye ngome za nafsi zao. Mtazamo wake kama mwandishi ni kwamba, jamii imepiga hatua katika juhudi za kumjengea mwanamke ujitambuzinafsia chanya ingawa bado vita dhidi ya kumdhulumu mwanamke katika hali na mazingira yote vinaendelea ili kuhakikisha kwamba, mwanamke hapembezwi zaidi katika jamii. Mtazamo wa Momanyi unatofautiana na wa Babu anayeonyesha kwamba, mwanga wa kujitambua na kupigania nafasi stahiki katika jamii bado ni hafifu. Watoto wasichana na wanawake wanaikubali hali yao jinsi ilivyo. Hii inatokana na ule uwezo mkuu wa mila na desturi za utamaduni jadi na urengwaji wao na mfumo wa Ki-Ubabedume unaomfanya mwanake aamini hali yake, ndiyo majaliwa yake na hawezi kwa vyovyote vile, kuibadilisha..

Tofauti nyingine kati ya kazi za Babu na Momanyi inajitokeza katika hatua inazochukua jamii katika kumjengea mwanamke ujitambuzinafsia chanya. Momanyi katika'Ngome ya Nafsi'(2004) na *Tumaini* (2006), anapendekeza mshikamano wa jamii katika kumjengea mwanamke ujitambuzinafsia chanya. Kwa mujibu wa nadharia yetu, jamii inahitaji kuungana kwa wanaume kwa wanawake ili kupiga vita ada ambazo zinamdhalilisha mwanamke na kuhakikisha hapembezwi. Hoja hii inabainika kupitia jitihada za jamaa wa Shabani kupigania haki ya Tumaini.

Mbali na kumpa makao, wanavunja kikao kilichoandaliwa na Mzee Masumbuko cha kupokea posa ya Tumaini. Msimamo wao ni ni kumkinga na kumlinda mtoto msichana dhidi ya mila zilizokuwa na uwezo wa kumkatizia masomo yake.. Tunasoma, '*Yaani Masumbuko umeleta*

*wageni hawa kutoka-sijui wapi Mambrui– kumposa mtoto wetu mchanga anayesoma shule? Hii ni aibu gani?*'

Kwa muktadha wa dondoo hili, tunaona jinsi jamii imejitahidi kupigania haki za mtoto msichana. Momanyi anathibitisha kwamba, jamii iko radhi kumpa msichana na mwanamke haki na hasa ya masomo. Ndoa za mapema ni majowapo ya mila potovu ambazo zinapigwa vita. Hivyo, jamii haitazami tu jinsi mtoto msichana anajengewa utambuzinafsia hasi ila inampigania ili kumjengea staha zaidi katika jamii. Tunaweza kusema kwamba, bado jamii haijafikia usawa wa kijinsia. Mbali na hayo, Ofisi ya D.O inampigania Tumaini baada ya jina lake kuondolewa katika orodha ya wanafunzi waliohitaji ufadhili wa kimasomo. D.O anakashifu kitendo cha chifu Andrea cha kumpembeza Tumaini kwa kusema; '*This is bad, really bad'* … Bwana Chifu, ningependa utwambie kwa nini umeleta majina ya wanafunzi wanne badala ya watano… (uk. 102).

Kauli hii ya D.O inabainisha jinsi asasi za kiserikali zilivyojizatiti kumhakikishia mwanamke haki yake. Hali sawa na hii inadhihirika pale ambapo Bi. Jeni ('Ngome ya Nafsi') anajenga makao ya wasichana wanaotoroka dhuluma dhidi yao katika jamii. Kwa jumla, Momanyi amefaulu kuonyesha jinsi jamii inavyoungana kumjengea mwanamke ujitambuzinafsia chanya. Mila potovu zinakashifiwa na kupigwa vita. Jamii imeshawishika kumwezesha mwanamke kujiendeleza. Mtazamo wa Momanyi unawatia ari wanawake na hasa wasichana kupigania nafasi yao katika jamii.

Kwa upande wa kazi za Babu, tunaona kwamba jamii anaiyolenga bado imeathirika na mtazamo jadi kumhusu mtoto-msichana.Tunafahamishwa kuwa mbali na Kibibi kuibuka mwanafunzi bora tarafani, ananyimwa nafasi ya kuendeleza masomo. Mwalimu Selemani hachukuliwi hatua za kisheria kwa kumnyima mtoto msichana haki ya kimasomo. Tunaona hata mwalimu wake mkuu, pamoja na afisa wa elimu tarafani, wanajaribu kumshawishi Mwalimu Selemani kwa upole tu bila kutumia vifungu vya sheria ya elimu vinavyoweza kumlazimisha kubadili msimamo huo wake. Isitoshe, katika *Heri Subira* (2010) , Sabra anaozwa mapema bila ya babake kupingwa kwani ni kawaida katika jamii yake kwa wazazi kuwapangia watoto wao ndoa. Wanaufeministi wanapinga ndoa za mapema kwani ni kinyume na haki ya mtoto msichana..

Ingawa mwanamke anashika hatamu katika harakati hii muhimu, bado anapingwa kwa kuchukuliwa kuwa hafai kwa misingi ya ukalautala wa nafasi yake kuwa finyu na funge katika jamii. Mhusika Mama Bintifundi anasaili... '*Tangu lini tukawa na maafisa wanawake hapa kwetu? Hicho ni kioja..kwake, wazo la kumhusisha mwanamke na kazi za afisini lilimtia kero kwani hastahili kabisa kutwaa madaraka kama hayo*'...(uk. 33). Kauli hii ni kichocheo kwa mwanamke anayejitambua kupigania nafasi yake ili aweze kuchangia kikamilifu kwenye ujenzi wa jamii yake katika utunzaji wa mazingira na hata kiuchumi. Wanaufeministi wanatoa mwito kwa wanawake kuungana kama kundi linalodhulumuiwa ili kushinda vita dhidi ya upembezwaji wao

Vilevile, Babu anajiegemeza kwenye masuala ya kijamii bila kujikita kwenye uongozi wa mwanamke kama anavyofanya Momanyi katika riwaya ya *Nakuruto*. Mbali na kutoa mchango wake kuhusu udhalilishwaji wa mwanamke kielimu na kindoa, ameangazia suala la mahari kwa njia mwafaka. Anakosoa wale wazazi wanaowachukulia wasichana wao kama vitega uchumi.

Hii ni kwa sababu wanabadilisha dhima ya mahari kwa msingi wa kiutamaduni. Ulipwaji wa mahari ulichukuliwa kama njia ya kutoa shukrani kwa wazazi wa msichana kwa malezi aliyopewa na wazazi wake. Ijapokuwa hivyo, kule kuweka kiwango cha juu cha mahari ni njia ya kumdhalilisha msichana kwa kuwa ni kumuuza kama bidhaa. Thamani ya binadamu haiwezi kumithilishwa wala kutosheleshwa kwa kitu chochocte kile. Babu anatoa taswira ya wazazi waliopoteza mwelekeo kuhusu suala la mahari. Lazima anayeoa alipe mahari inayolingana na malezi pamoja na huduma nyinginezo alizopewa msichana. Mama Amali anauliza… '*utaweza mahari*... Heshima ya mtu binafsi inapotea. Mahari yanarutubisha utumwa kwa mwanamke. Kama milki ya mumewe, anatakiwa kumtii mumewe bila swali na kunyenyekea mbele zake kila wakati kama mtumwa.

**Ulinganifu wa Uwasilishaji wa Mazingira ya Jamii Katika Kukuza Maudhui ya Upembezwaji ya Mwanamke Kati ya Kazi za Clara Momanyi na Omar Babu**

Waandishi Momanyi na Babu wameangazia namna ambavyo mazingira ya utunzi yanavyoathiri maudhui katika kazi zao. Kwa mujibu wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, jamii inahitaji kuungana na kupiga vita mila na desturi kandamizi kwa mwanamke. Jambo hili likitekelezwa, mwanamke ataweza kujiamini na kupigania nafasi yake katika jamii kama wanavyosema Njogu na Chimerah (1999) kwamba, mwanamke ana uwezo wa kufikiri na kufanya kazi kwa bidii ili kunafasika sawa na mwanamume katika jamii. Mtazamo huu wa wanaufeministi unakosa kuzingatiwa katika mazingira ya jamii wanazolenga Babu na Momanyi. Wanaonyesha kwamba, utamaduni jadi na mfumo wa Ki-Ubabedume umemdidimiza mwanamke na kumnyima nafasi ya kujiendeleza kielimu.

Katika Momanyi (2004 na 2007 zitaje kazi husika) mwanamke anafungwa pingu za utamaduni kandamizi ambao umetawala jamii ya kazi hizi mbili. Katika jamii anayolenga Momanyi, mwanamke anadhalilishwa kwa kulazimishwa kutekeleza ada ambazo hazifai kwa mujibu wa kipindi cha utunzi wake (karne ya ishirini na moja). Ada hizi ni tohara na ndoa za mapema tena za kulazimishiwa wachumba. Mhusika Naseko anakejeliwa na wanawake kwa kuambiwa, '*Kilio ni cha nini sasa? Binti akisha kukoshwa unyago ya nini kumweka nyumbani? Hana budi aende kwa mumewe*'... (uk. 101). Mazingira ya utunzi yamefungamana na mila na ada kandamizi kwa mwanamke. Mwandishi anafafanua jinsi kizazi cha watoto wasichana na wanawake kinaangamizwa kwa kuigizwa katika ndoa za mapema.

Momanyi anatuelea jinsi wasichana wadogo wanavyotatizika kiuzazi baada ya ndoa za mapema. Jambo hili linadhihirika kupitia mke wa nne wa Mzee Sakaja katika 'Ngome ya Nafsi' (2004) na mmoja wa dadake zake Tumaini katika *Tumaini* (2006) anayeozwa kwa lazima. Mazingira ya aina hii ndiyo yanayopigwa vita na wanaufeministi ili kumhakikishia mwanamke uhuru wa kujiamulia mambo yake na kujiendeleza bila kushinikizwa kuzingatia mila potovu. Momanyi amefaulu kuonyesha pengo lililopo katika kumjengea mwanamke ujitambuzinafsia chanya ili kujizatiti zaidi kupambana na udhalimu dhidi yake. Babu hajaachwa nyumba kuangazia athari za mazingira ambayo yanatawaliwa na mfumo wa Ki-Ubabedume na mila zilizopitwa na wakati. Kupitia kwa msimamo wa jamii wanazolenga, mwanamke anakandamizwa kwa kunyimwa nafasi ya kujiendeleza kielimu. Badala yake, anapangiwa ndoa za mapema zinazomletea maudhi maishani.

Mwanamume amepewa mamlaka ya kuitawala familia yake na kuamua kuhusu mambo yote anayoona mwafaka kwa mkewe na watoto wake. Tunamwona Sabra akipangiwa ndoa angali mdogo. Hivyo, Babu na Momanyi wanalenga mazingira yanayofanana ya jamii inayotawaliwa na desturi kandamizi kwa mwanamke. Isitoshe, kwa mujibu wa mazingira ya utunzi, Babu na Momanyi wamefaulu kuonyesha nafasi ya mwanamke katika asasi ya ndoa. Wamitila (2002: 157) `anaieleza ndoa kama asasi ya kitamaduni inayoendeleza upembezwaji wa mwanamke. Anazidi kudai kwamba, asasi hii inajenga dhana kwamba, mwanamume ana uwezo mkubwa akilinganishwa na mwanamke.

. Mazingira ya kiutamaduni humpa mwanamume uwezo na mamlaka wa kuiongoza familia yake. Mwanamke haruhusiwi kumkata kauli mumewe. Momanyi (2006) anasema,

> Bi Amina hakutaka kuivunja nyumba yake kwa kwa kumfanyia mumewe vitimbi… Aliahiari shingo upande kuvumilia unyanyaswaji huo akakubali bila hiari yake kutiwa shemere, na kuwa tutwe mbele ya mumewe ilimradi awalee wanawe na kuisitiri nyumba yake… (uk. 13).

Mwandishi anaonyesha jinsi mazingira yanavyomfanya mwanamke kujinyenyekeza na kukosa satua mbele ya mumewe. Tabia kama hii inamfanya mwanamume kumtawala na kumdhalilisha. Ni bayana kwamba, jamii haitambui nafasi ya mwanamke katika kutoa maamuzi kuhusu familia yake. Daima hoja za mumewe ndizo zinastahili kuzingatiwa. Babu anaonyesha mazingira kandamizaji kwa mwanamke kwa kuonyesha jinsi jamii inavyomtarajia mwanamke kujiweka kadiri afanyavyo Momanyi. Kupitia kwa mamake Sabra tunapata nafasi ya mwanamume katika ndoa kama anavyomtahadharisha Sabra kwa kumwambia;.. ‘*Mume ndiye kichwa cha nyumba. Hadhari kubishana naye*’*…* (*Heri Subira*, 2010, uk. 44). Katika *Kala Tufaha* (2017), Babu analiangazia suala la mazingira ya jamii kuhusu nafasi hasi anayopewa mwanamke katika ndoa. Mamake Kibibi anamkumbusha kuwa ni lazima ajinyenyekeze kwa mumewe. Anamwambia, ‘*Mumeo ni dume. Si gumegume…Mbembeleze daima. Akikwita labeka! Mlevye kwa mahaba*’*…* (uk. 17). Kauli hizi zinaashiria mazingira kandamizi kwa mwanamke katika jamii. Hii ndiyo sababu inayowafanya Wanaufeministi wayatilie maanani mazingira anamoishi mwanamke, wanapopinga udhalimu kwa mwanamke hasa anapotiwa kimya cha lazima. Hivyo, ni wito unaotolewa na waandishi Momanyi na Babu kupigania haki za mwanamke katika ndoa.

Kuna ulinganifu katika mazingira ya nyumbani kati ya kazi za Babu na Momanyi. Katika *Tumaini* (2007), Momanyi anaangazia mazingira ya nyumbani kwa Chifu Andrea ambayo yanachangia upembezwaji wa mwanamke kwa kuchukuliwa kama chombo cha kumstarehesha mwanamume. Chifu Andrea na mwanawe Majuto kwa pamoja, wanajaribu kumbaka Tumaini. Sawia na hayo, Kibibi anabakwa na Fumbwe anapomfanyia kazi ya uyaya nyumbani kwake. Suala hili la ubakaji linajitokeza katika kazi za Momanyi na Babu mtawalia. Inabainika kwamba, mazingira ya nyumbani wanakoajiriwa kazi ya uyaya wasichana na wanawake, yanachangia katika kueneza hali ya ujitambuzinafsia hasi kwa mwanamke. Waandishi hawa wanatoa tahadhari na kuwahimiza wajakazi kuwa makini zaidi ili kujiepusha na dhuluma ya ubakaji na maovu mengine dhidi yao pindi wanapokuwa kazini.

**Tofauti Kati ya Uwasilishaji wa Mazingira Katika Kazi za Omar Babu na Clara Momanyi**

Waandishi Omar Babu na Clara Momanyi wana mielekeo tofauti katika kubainisha jinsi ambavyo mazingira yanachangia katika maudhui ya ya ujenzi wa ujitambuzinafsia wa jinsia katika kazi zao. Wahusika wa kike katika kazi mbili za Momanyi 'Ngome ya Nafsi' na *Tumaini* wanapembezwa kwa kulazimishwa kutekeleza ada za kijamii zikiwamo ukketwaji, ndoa za mapema na za lazima, ubaguzi katika maendeleo ya kijamii pamoja na udhalilishwaji kingono. Mila hizi humzuia mwanamke kuafikia ujitambuzinafsia chanya. Mhusika Tumaini anajikuta katika utamaduni duni wa ndoa za mapema na kupashwa tohara ambao humpi nafasi ya kuafikia ndoto yake ya kimasomo. Anapinga mikakati anayowekewa na jamii yake. Tunampata Tumaini akisimama kidete na kumwambia mamake, '*...ikiwa unayotaka kunieleza yanahusu tohara, mama sahau- sahau kabisa maana nilisema tangu kitambo kuwa mila kama hiyo ni ya kizamani, ni ya kikatili na kishenzi....*' (uk 16).

Tumaini anafahamu kuwa akishapashwa tohara, litakalofuatia ni kuozwa kwa mtu asiye chaguo lake. Ni mpango unaoenda kinyume na shauku yake ya kujijengea ujitambuzinafsia chanya kupitia azimio lake la kusoma na kuwa daktari. Tumaini anajikomboa kwa kutorokea kwa mamake mdogo ambako anafasika kuendeleza masomo yake kadri anavyozaimia. Hali kama hii inampata Naseko anayeozwa kwa Mzee Sajaka ambaye pia kama Tumaini, anafanikiwa kutoroka na kupata makao mapya kwa Bi. Tesi.

Tumaini anapojiunga na shule mpya, mazingira ya shuleni mle yanamwathiri kwa kiasi kikubwa. Anabezwa na kuonekana 'Mwingine'. Wavulana watundu ndio wanaoongoza bezo na stihizai hizo kwa kuwa tu alitoroka kwao. Kutotimiza ada za jamii yake kunamfanya anyanyapazwe na wenzake. Mfano mwema ni jinsi Kijungwe anavyomkejeli kwa kumwambia maneno ya kumuudhi. Tofauti na Momanyi, mazingira anayolenga Babu yamejikita kwenye ada za ndoa za mapema ambako mwanamke hana uwezo wa kujiokoa wala kujikomboa pindi tu dhuluma dhidi yake zinapoanza. Hii ndiyo sababu Sabra akaozwa Khalidi ambaye si chaguo lake. Wahusika wa Momanyi (wasichana wadogo) wamedhihirisha wana uwezo mkubwa wa kujiamulia wanalotaka maishani na kisha kulitimiza. Ni wahusika watambuzi ambao wana lengo la kubadili mkondo wa maisha yao tofauti na wanavyotakiwa wafanye kulingana na tamaduni za jamii zao. Kwa upande mwingine, watoto wasichana wa Babu wanafuata maagizo ya wazazi hata kama yanakinzana na malengo yao. Baada ya kutumbukia kwenye dhiki, ndipo wanafunguka akili na macho na kuanza safari mpya ya kujipigania nafasi na ujitambuzi wao stahiki katika jamii. Mfano ni Sabra na Kibibi. Wanajitambua tu baada ya 'kufunzwa na ulimwengu.'

Tofauti na mazingira tulivu kwa mtoto wa kike na mwanamke katika bunilizi za Momanyi, Babu hajikiti au kuonyesha mazingira mbadala kwa mtoto wa kike na mwanamke ijapokuwa anawasawiri wakiwa katika hali zisizoridhisha. Mazingira ambamo Babu anawatia wahusika wake ni finyu na kandamizi kwa ujenzi wa ujitambuzi chanya kwa jinsia ya kike. Ikiwa nyumbani kwao hakumfai, hakuna pengine angeweza kupata usaidizi. Kwa mfano, Mwalimu Selemani anapompembeza Kibibi kimasomo, Kibibi anasalia papo hapo nyumbani na kuzidi kunyanyaswa na hatimaye, akakosa kabisa nafasi ya kusoma zaidi. Anabakia katika mamlaka ya babake anayemtafutia kazi ya uyaya. Isitoshe, babake anampangia ndoa ambayo Kibibi mwenyewe anaishabikia. Ni dhahiri kuwa mazingira kama haya, yanakiangamiza kizazi cha kike na hasa cha wasichana wa umri mdogo. Badala ya kusoma na kushiriki kwenye maendeleo ya

kijamii, msichana analazimika kuishi maisha ya kizamani kama walivyoishi wazazi wake zama zao.

Tofauti nyingine inayodhihirika katika mazingira wanayoyalenga waandishi Babu na Momanyi, ni athari ya mazingira ya asasi za utawala na maofisa wa utawala. Momanyi na Babu wanatofautiana kwa namna wanavyowawakilisha na kuwasawiri Chifu Andrea na Fumbwe (ambaye ni mkuu katika kikosi cha polisi), na mitazamo yao hao wawili kumhusu mwanamke. Mazingira haya mawili yanapelekea mwanamke ajikute katika hatari ya aidha ya jaribio la au kubakwa hasa na mwanamume. Babu anaonyesha jinsi Fumbwe anavyofaulu kumbaka Kibibi na kumpa ujauzito. Kinyume na hali hii, mhusika Tumaini katika *Tumaini* (2006), anafanikiwa kujiokoa kwa kutumia akili na uwezo wake ukiambatana na dhamira angavu na ujasiri mkubwa. Steady (1981) akinukuliwa na Njogu na Chimerah (1999), anasema kuwa mwanamke ni lazima atumie akili yake kujijengea ujitambuzinafsia chanya.

Ijapokuwa Kibibi na Tumaini wanakumbwa na changamoto zinazolingana, Tumaini anaonyesha ujasiri na ufanisi katika kujinasua kutoka kwa mtego mikononi mwa mwanamume. Momanyi anaonyesha kwamba, mwanamke ana uwezo wa kutumia akili yake kujikomboa kutokana na baadhi ya dhuluma zinazoelekezwa kwake na wanaume kutokana na taasubi zao za kiume; kwamba, wana uwezo na mamlaka juu ya wanawake na jinsia ya kike kwa jumla. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inaunga mkono ujasiri na ushujaa wa mwanamke katika harakati za kujijengea hadhi na ujitambuzi wake katika jamii.

Momanyi anaonyesha kwamba, mbali na changamoto anazopitia mwanamke, ana nafasi ya kujikomboa na kujijengea ujitambuzinafsia chanya katika jamii. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inatambua kwamba, mwanamke anaweza kujikomboa na kuishi bila kudhulumiwa. Ukombozi wa Tumaini unapatikana anapofaulu katika masomo na kujiunga na chuo kikuu ambayo imekuwa ndoto yake tangu mwanzo wa riwaya. Momanyi amefaulu kuonyesha kwamba, mbali na mazingira kandamizi, mwanamke anaweza kuafikia ndoto zake ilmuradi atajitahidi na kupigania haki yake.

Babu kwa upande wake, anaonyesha kwamba mwanamke hawezi kujiendeleza kimasomo. Kizingiti kikuu kinachomtinga mwanamke ni mazingira finyu yaliyochangamana na itikadi potovu kumhusu mwanamke katika kupenya na kuyaelewa mazingira hayo kandamizi na kujitahidi kujikomboa. Ndiyo sababu wahusika wake Kibibi, Sabra na Amali wanafedheheshwa na mwanamume kwa kuzingatia mtazamo hasi wa mazingira ya jamii zao. Babu anatambua uwezo wa mwanamke wa kuinuka baada ya kushindwa kupenya mazingira yake. Hii ndiyo sababu anaangazia suala la ufanisi wa mwanamke katika biashara. Tunaweza kusema kwamba, Babu anamhusisha mwanamke na biashara ya kuuza sandarusi na makaa. Vilevile, biashara ya mkahawa. Hatambui nafasi ya mwanamke katika kujipatia elimu na kushiriki katika ujenzi wa taifa katika ngazi za juu katika jamii. Namna haonyeshi mwanamke na mwanamume wakishirikiana pamoja katika kazi za hadhi kama vile udaktari, utawala na nyinginezo.

Mtazamo wa Babu unapingwa na Wanaufeministi kwani wanatambua uwezo alio nao mwanamke ambao ni sawa na wa mwanamume katika maendeleo ya jamii. Momanyi katika *Tumaini* (2007), ameangazia athari za mazingira ya malezi, shuleni na utangamano wa jumla katika jamii katika kumzindua mwanamke na kumpa ari ya kupinga upembezwaji wake. Njogu

na Chimerah (1999) wanapendekeza pawe na muungano wa wanawake kama kundi na kupigania nafasi zao katika jamii. Kwenye muktadha huu, tunamwona Bi. Amina akizinduka na kubadili nia yake ya kumsukumiza Tumaini kutekeleza matakwa ya babake.. Tunasoma,

> ‘Kwa nini mwanangu huyu mdogo mwenye umri wa miaka kumi na minne tu aolewe? Kwa nini akatiziwe masomo ilhali ana ari ya kusoma? Kwa nini amsukume kwenye ndoa ya mapema…? Kwa nini mwanangu anadiwe kama bidhaa inayomwozea muuzaji?’ (uk. 35).

Maswali anayosaili Bi. Amina ni ya mwanamke anayetambua nafasi yake kama mzazi. Anapinga kauli ya mumewe ya kumpembeza binti yao mdogo kwa kumpangia ndoa ya mapema. Mazingira yamemfungua macho akathamini msimamo wa binti yake wa kuendelea kusoma naye anaamua amuunge mkono. Mchango wa mawazo na hamasa kwa dada yake ndio unamfanya Bi. Amina kuungana na wanawake wanaopinga mila kandamizi dhidi ya mwanamke. Bi Amina anazidi kuelekeza, ‘*Sasa nimeona nafsi yangu, sihitaji kuonyeshwa*’ … (Uk. 3*).* Momanyi amefaulu kuangazia jinsi mwanamke anavyoweza kubadilisha msimamo wake kulingana na mazingira yake na kukwepa hali zote zinazoweza kumjengea ujitambuzinafsia hasi katika jamii. Kubadili nia na mtazamo kwa Bi. Amina ndiko kunamfanya amhimize bintiye kutia bidii katika masomo. Ni himizo hili analolipata kwa mamake linalomfanya afaulu vyema katika masomo yake.

Tatizo kuu na la kimsingi linalodhihirika katika kazi za Momanyi, ni jinsi wahusika muhimu kama Mzee Mengo (‘Ngome ya Nafsi’) na Mzee Masumbuko (*Tumaini*)*,* ambao ni wanaume wakuu na wenye ushawishi mkubwa kama mawakala wa utamadunu jadi na Ubabedume, wasivyobadilika kamwe; kimsimamo na kimtazamo, kuanzia mwanzo wa kazi hizi hadi mwisho. Tunaweza kudahili kuwa, itakuwa vigumu kwa mtoto msichana, mwanamke na jinsia ya kike kwa ujumla, kuweza kujijengea ujitambuzinafsia chanya pasina mazingira mwafaka. Wanaufeministi wanaamini ukombozi wa mwanamke na jinsia ya kike utafaulu zaidi endapo jinsia hizi mbili zitaungana ili kufanikisha mabadiliko yenye maana na endelevu. Na hapo ndipo waandishi hawa wanafeli japo Babu, anaelekea kuonyesha pana matumaini kwani tunawaona wanaume (*Kala Tufaha* na *Heri Subira*) wakiungana na wanawake katika kuteteta haki zao na kupinga upembezwaji wa mwanamke kwa misingi ya jinsia yao.

Tofauti na Momanyi, Babu hajalenga mazingira ambayo yanaweza kuathiri msimamo wa mwanamke hasa katika ndoa. Anatuchorea picha ya mwanamke asiyeweza kupinga amri potovu za mwanamume kuhusu familia yake. Analenga mazingira ambayo yanamlazimisha mwanamke kuendeleza itikadi za unyumba alizofunzwa kupitia utamaduni. Katika *Kala Tufaha* (2007),tunamwona Bi. Khadijah analia tu baada ya kugundua kuwa bintiye ni mja mzito. Anasaili,

> ‘Aibu gani hii mwanangu? Mbona unatutia izara?... Babako utamwambia nini? Unataka tuuawe mwanangu?... Wooi! Mama yangu wooh!Mimi nitamlilia nani? … (uk. 89).

Ingawa Kibibi anamweleza kilichomsababishia ujauzito, Bi. Khadija haelewi. Anazidi kumlaumu. Ingelikuwa Bi. Khadijah anafahamikiwa na hali ya jamii yake, angemshawishi mumewe kumchukulia Fumbwe hatua kwa kumchafua mtoto wao. Babu analenga mazingira finyu yasiyompa mwanamke nafasi ya kuzinduka na kupigania haki yake katika jamii. Wanaufeministi wanapinga mazingira kama hayo na kupendeza watunzi wa kazi za sanaa kuwa na wahusika wa kike walio vielelezo.

**Hitimisho**

Katika sehemu hii tumeona kwamba, kuna ulinganifu na ulinganuzi wa kiasi cha haja kati ya kazi za Babu na za Momanyi katika kushughulikia maudhui ya ujenzi wa utambulizinafsi wa jinsia katika kazi zao. Imebainika kwamba, kuna uwiano fulani katika usawiri wa wahusika wao. Wote Babu na Momanyi, wamewasawiri wahusika wa kike wanaopembezwa kufuatia taasubi za kiume zinazotiwa nguvu na utamaduni jadi na mfumo wa Ki-Ubabedume. Isitoshe, mazingira ambamo watoto wasichana na wanawake wanazaliwa, kulelewa au kuolewa, ni pingamizi kuu katika kumpa mwanamke nafasi stahiki katika jamii. Ingawa mwanamke anakumbana na pingamizi hizi, bado ana nafasi ya kupigania nafasi yake na kuibuka mshindi. Hili limejitokeza kupitia kwa wahusika wakuu wa kike katika kazi za watunzi Babu na Momanyi.

**MAREJELEO**

Babu, O. (2007). *Kala Tufaha*. Nairobi: Oxford Publishers.

Babu, O. (2010). *Heri Subira*. Nairobi: Oxford Publishers.

Bank, O. (1990). *Faces of Feminism. A study of Feminism as a Social Movement*. Basil Blackwell: USA.

Chacha, W. C. (2013). 'Taswira ya mwanamke katika tamthilia za Nguzo Mama na Mama*Ee'*. Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapioshwa.)

Chesaina, C. (1987). 'Women in African Drama: Representation and Role'. Tasnifu ya Uzamifu, University of Leeds. (Haijachapishwa).

Kamwara, K., (2022). 'Ujenzi wa Ujitambuzinafsia wa Jinsia na Upembezwaji wa Mwanamke katika Bunilizi za Clara Momanyi na Omar Babu. Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu cha Nairobi,. (Haijachapishwa

Kamwara, K., (2016). 'Mtazamo Mpya katika Sauti ya Kike katika Riwaya ya Kiswahili'. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Mount Kenya. (Haijachapishwa).

Mboya, L. A., Mohochi, E. S., & Kisurulia, S. (2018). 'Dhuluma kama Kichocheo cha Mzinduko wa Wanawake katika Riwaya ya Kiswahili'. Rongo: Rongo University Press. (http://respository.rongovasity.ac.ke/handle/123456789/1860).

Mikell, G., (1997). *African Feminism: The Politics of Survival in Sub-Sahara Africa.*

Mji?: University of Pennsylvania Press.

Mohochi S., et. (2018). 'Dhuluma kama Kichocheo cha Mzinduko wa Mwanamke katika Riwaya ya Kiswahili'. Makala ya Chuo Kikuu Cha Rongo.

Momanyi, C. (2006). *Tumaini.* Nairobi: Vide-Muwa publishers.

Momanyi, C. (2009). *Nakuruto*. Nairobi: Longhorn publishers.

Musyoka F. M. (2011). 'An Analysis of the Woman in Gender Role-Play Dynamics in Kenyan Kiswahili Drama.' Tasnifu ya Umahiri. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa.)

Hamadi, M. (9.7.2019). 'Mwanamke Bomba' (Msururu wa Vipindi vya Televisheni vya 'Citizen Kenya"). (https://youtu.be/FrBDtjx_SM).

Swaleh, A. (2011). 'A Critique of the Mapping and Construction of Gender Identity and Authority in Selected Kiswahili Novels'.Tasnifu ya Umahiri. Chuo Kikuu cha Nairobi. \

Wafula,R.M.naK. wa Njogu(2007).*NadhariazaUhakikiwaFasihi.*Nairobi:Jomo KenyattaFoundation.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi; Nadharia na Mbinu.*Nairobi: Phoenix Publishers.